

Nipashe Jumanne 12, 2026 Pg 4

Ajali nyingine yaua wawili, 13 wajeruhiwa Iringa

Na Waandishi Wetu

ZIKIWA zimepita siku nne tangu kutokea kwa ajali ya basi na lori katika eneo la Kijiji cha Tanangozi, Kata ya Mseke, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na kuua watu watano, ajali nyingine imetokea mkoani humo na kuua watu wawili.

Ajali hiyo imetokea jana ikihusisha basi la abiria la Kampuni ya Classic linalofanya safari zake kati ya Harare nchini Zimbabwe na Jiji la Dar es salaam baada ya kugongana uso kwa uso na lori.

Ajali hiyo ilitokea jana katika eneo la Mseke Barabara Kuu ya Iringa-Mbeya ambapo baada ya magari hayo kugongana basi lilitumbukia mtoni.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, Dk. Alfred Mwakalebela alisema walipokea majeruhi 13 ambao kati yao watatu ni wanawake na wanaume ni 10.

Dk. Mwakalebela alisema majeruhi watatu wako katika hali ya mahututi, akiwemo mjamzito aliyevunjika mgongo, mwingine amejeruhiwa mbavu na kutokwa



Wakazi wa Kata ya Mseke katika Wilaya ya Iringa, mkoa wa Iringa, wakitazama basi la kampuni ya Classic linalofanya safari kati ya Harare, Zimbabwe na Dar es Salaam Tanzania lililotumbukia kwenye mto Msimu uliopo kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa baada ya kugongana na lori jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

damu ndani ya kifua, huku mwingine akiwa amevunjika kawaida.

Alisema kuwa majeruhi wote 13 wamelazwa katika hospitali hiyo kwa uangalizi maalum wa madaktari.

"Kati ya wale waliofariki, mmoja ni mtanzania anayeripotiwa kuwa anaishi katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe ambaye ametambuliwa, lakini majeruhi wanne ni raia wa Zambia na raia wanne wa Zimbabwe," alisema Dk.

Mwakalebela.

Dk. Mwakalebela alisema hali za majeruhi zinaendelea kufuatiliwa na baadhi yao huenda wakaruhusiwa kutoka kesho kutwa endapo hali zao zitaimarika.

Wakizungumza na gazeti hili, mmoja wa majeruhi kwenye ajali hiyo, Mbaraka Hassan mkazi wa Tanga alisema alipanda basi hilo kutoka Zimbabwe na alikuwa anarejea nyumbani.

Alisema ilikuwa majira ya asu-

buhi na mapema na wengi walikuwa wamelala na kwamba aliposikia kishindo kikubwa ghafla akajikuta korongoni.

"Mimi ni dereva wa IT (magari ya yaendayo nje ya nchi) nasafirisha magari madogo kutoka Dar es salaam kwenda katika nchi mbalimbali ikiwemo Zimbabwe, nilikuwa narudi nyumbani Tanga kupitia Chalinze," alisema Hassan.

Naye Elias Sinkala ambaye ni raia wa Zambia alisema alipanda

Wiki iliyopita watu watano walifariki dunia papo hapo na wengine 28 kujeruhiwa kufuatia ajali mbaya ya barabarani iliyohusisha basi la abiria pamoja na lori la mizigo lililokuwa limebeba vinywaji baridi.

Ajali hiyo ilitokea katika eneo la Kijiji cha Tanangozi, Kata ya Mseke, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, majira ya saa nane kasoro usiku, baada ya magari hayo kugongana uso kwa uso.

Imeandaliwa na Friday Simbaya na Flora Kamaghe (Iringa)

CS CamScanner

Wawili wafa basi likigongana na lori Iringa

Na Frank Leonard, Iringa

WATU wawili wamekufa na wengine 13 kujeruhiwa baada ya basi la Kampuni ya Classic kugongana na lori katika eneo la Mseke wilayani Iringa.

Basi hilo lililokuwa likifanya safari kati ya Harare, Zimbabwe na Dar es Salaam,

Tanzania liligongana uso kwa uso na lori na kisha likapinduka na kutumbukia korongoni katika Barabara Kuu ya Iringa-Mbeya.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, Dk Alfred Mwakalebela alisema hospitali hiyo ilipokea majeruhi 13, wakiwamo wanawake watatu na wanaume 10 na wote walikuwa wakipatiwa

matibabu kwa uangalizi maalumu wa madaktari.

Dk Mwakalebela alisema majeruhi watatu walikuwa katika hali mahututi akiwemo mjamzito aliyepata jeraha kubwa mgongoni.

Alisema majeruhi mwingine aliumia mbavu na damu kuvujia ndani ya kifua huku wengine wakipata mivunjiko na majeraha.

"Tunawafuatilia kwa

karibu majeruhi wote waliolazwa na endapo hali zao zitaendelea kuimarika, baadhi yao wanaweza kuanza kuruhusiwa kuanzia kesho kutwa," alisema Dk Mwakalebela.

Kwa mujibu wa taarifa za hospitali, mmoja wa walio-kufa ametambulika kuwa ni mkazi wa Tunduma huku majeruhi wakijumuisha raia wanne wa Zambia na wanane

wa Zimbabwe.

Magari hayo yamegongana ikiwa ni wiki moja tu tangu kutokea kwa ajali nyingine iliyohusisha basi la Shabiby lililokuwa likitoka Dodoma kwenda Mbeya.

Basi hilo liligongana uso kwa uso na lori katika Kijiji cha Tanangozi, Kata ya Mseke na kusababisha vifo vya watu sita huku wengine 28 wakijeruhiwa.

Katika hatua nyingine, Dk Mwakalebela alizungumzia pia majeruhi wa ajali iliyohusisha basi la Shabiby na lori akisema majeruhi wawili bado wanaendelea kupatiwa matibabu hospitalini hapo.

Alisema mmoja wao alikuwa akimaliziwa kushonwa jeraha la jicho huku mwingine akitarajiwa kufanyiwa upasuaji kutokana na mivunjiko aliyopata.